UHURU Ijumaa Desemba 12, 2025

Pg 16.

yatakayobainika kukwepa kutoa tiketi hizo yatatozwa faini

# LATRA yatangaza msako wamiliki wa mabasi wanaovunja sheria

**Shinyanga**
**SALVATORY NTANDU**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA) mkoani hapa imetangaza msako mkali kwa watoa huduma za usafirishaji watakaobainika kukwepa kutoa tiketi za kieletroniki na kuzidisha abiria.

Kauli hiyo ilitolewa na Ofisa Mfawidhi wa LATRA Mkoa wa Shinyanga, Denis Maghembe, katika msako maalum wa kukagua mabasi yanayotoa huduma ya kusafirisha abiria kwenda mikoani uliofanyika katika kituo kikuu cha mabasi mkoani hapa jana.

Alisema kwa mabasi yatakayobainika kukwepa kutoa tiketi hizo yatatozwa faini kwani wanaikosesha serikali mapato huku wakijua wazi kufanya hivyo ni kosa kisheria.

"Katika msako wa leo (jana) makosa tuliyoyabaini ni katika mabasi matano madogo ya abiria ambayo yalizidisha abiria na kutotoa tiketi za kieletroniki. Tumewatoza faini na wakirudia tutachukua hatua zaidi, tumejipanga kudhibiti vitendo hivyo viovu," alisisitiza.

Maghembe alisema msako huo utakwenda pamoja na ukaguzi wa watoa huduma ndani ya mabasi kama wamepatiwa mafunzo na kusajiliwa kwani ni takwa la kisheria ambapo utekelezaji wake ulikwishaanza.

Kwa upande wake, Peter Kisusi ambaye ni abiria alisema ili kudhibiti mabasi kutojaza abiria ni lazima elimu itolewe kwa wakatisha tiketi maana wao ndiyo sababu ya mabasi hayo kujaa.

"Nimetoka Simiyu nakwenda Mpanda, nimekata tiketi nimeambiwa nafasi zipo ila nimeigia katika gari naambiwa hakuna nafasi. Hii siyo sawa na unakuta unashida unalazimika kusafiri kwa kusimama au kukaa chini," alieleza.

Utingo wa basi kutoka kampuni ya Abood, Doris Godfrey alisema LATRA wanatoa mafunzo namna ya kuwahudumia abiria, hivyo ni muhimu kila mwajiri akatekeleza takwa hilo la kisheria ili kuboresha utoaji huduma bora za usafirshaji nchini.

"Nimepata mafunzo namna ya kumhudumia abiria akiwa ndani ya basi, ninawasihi wanaotaka kufanya kazi hizi ni lazima wakapate mafunzo kwanza kama sheria inavyotaka," alifafanua.